

Kuhusu MWONGOZO WA UTENDAJI wa SBS

SBS ni televisheni ya taifa iliyo huru, radio na huduma za mtandao vinavyowajibika kwa umma wa waustralia kama ilivyoelezwa kwenye **mkataba wetu**. Tunagharamiwa na serikali ya Australia na mapato yatokanayo matangazo.

Katika mtandao wetu tunatoa simulizi ya kiaustralia kama vile taarifa za habari za ndani na za kimataifa na mambo yanayojiri, michezo, michezo ya kuigiza ya kimataifa na simulizi, vyakula, filamu na huduma za radio kwa lugha zaidi ya 60. Sisi pia ni waanzilishi wa simulizi za mataifa makuu pamoja na televisheni ya watu asilia inayotoa programu ya matangazo kwa jicho la watu asilia.

Kuhakikisha maudhui yetu yanakidhi matarajio ya jamii, tuna Mwongozo wa Utendaji wa SBS, unaotoa kanuni na viwango vya maudhui yote ya SBS bila kujali ni wapi unayapata-kwenye televisheni, radio, mtandaoni ama kwenye mitandao ya kijamii.

Mwongozo wa Utendaji unazingatia mambo muhimu kama vile:



IMANI

Namna tunavyotoa maudhui yanayoamika na yanayoendana na mahitaji

- Tunafanya maamuzi huru yanayohusu maudhui yetu.
- Taarifa zetu na maudhui ya mambo yanayojiri ni sahihi, yenye uwiano na yasiyo na mlengo, na yenye maslahi ya taifa.
- Tunayapa nafasi maoni na mitazamo tofauti-maudhui yetu yanaweza kuwa bunifu na yanatoa changamoto ikiwa ni pamoja na yenye utata ama kuchochea hasira.



UWAZI

Namna tunavyokuongoza kuchagua maudhui

- Tunatoa taarifa ili uweze kuchagua maudhui yanayokufaa na watoto wowote na vijana walio chini ya uangalizi wako.
- Tunahakikisha matangazo yanajitenga na maudhui na tunaweka kanuni za namna ya kuweka aina fulani ya matangazo.
- Kwa aina ya maudhui yanayoweza kukarahisha, tunazingatia aina ya hadhira, tunazingatia umakini, kutoa tahadhari inapobidi, na tunaonyesha tu maudhui hayo pale yanapoendana na sera yetu ya uhariri.



HESHIMA

Namna tunavyozingatia heshima na kuidumisha




- Tunakwepa maudhui yanayohamasisha mitazamo potofu na ubaguzi ikiwa ni pamoja na kuzingatia muktadha.
- Tunatoa madhui katika lugha nyingine tofauti na Kiingereza pamoja na kuhamasisha maoni tofautitofauti.
- Tuko makini sana juu ya namna maudhui yahasuyo mambo ya watu asili yanavyotolewa na tunazingatia itifaki za Waaborijini na watu wa visiwa vya Torres Strait.
- Tunaheshimi faragha za watu, ambazo tunaziwekea uwiano na wajibu wetu wa kuhabarisha.



UWAJIBIKAJI

Namna tunavyowajibika

- Tunakupatia njia mbalimbali ambazo unaweza kutupatia mrejesho uhusuo maudhui na huduma zetu, uwe wa kutusifia ama kutukosoa.
- Tuna mchakato ulio huru wa kuwasilisha malalamiko chini ya Mwongozo wa utendaji, ambayo yanafanyiwa na mtu maalum aliyeteuliwa na SBS



Pata maelezo zaidi

sbs.com.au/aboutus/sbs-code-of-practice